114 IMBA habari njema: Mungu apenda wote

114

1. Imba habari njema: Mungu apenda wote! Uihubiri damu ituponyayo roho! Taja karama kubwa: Mwana alitujia, pasha habari hiyo kwa kila mtu!

> ***Pambio:***
> *Yesu msalabani alifilia wote, alitupatanisha na Mungu, Baba yetu. Pazia la hekalu likapasuka huko, njia imefunguka kwa wewe, nami!*

2.Uwaimbie wenye shida na sikitiko na wapigao vita katika majaribu! Imba katika miji, pasha habari njema: Yesu awatafuta kwa pendo kubwa!

3.Imba katika giza, lisipofika jua, uwaimbie wote, watu wa kila bali! Imba mapema sana, na adhuhuri pia, sifu Mwokozi hata usiku waja!

Elsa Eklund, 1918?